HOTUBA YA MHESHIMIWA MAMA SALMA KIKWETE

KATIKA ZAHANATI YA KITUNDA

TAREHE 28 APRILI, 2010

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ndugu William Lukuvi (Mb)

Mhe. Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ndugu Jordan Rugimbana

Mwenyekiti wa CCM, Mkoa Ndg. John Guninita

Mwenyekiti wa UWT Mkoa, Bibi. Zarina Madabida

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Dr. Nelson Mabruki

Mhe. Mbunge wa Jimbo la Ilala, Ndg. Musa Zungu

Mheshimiwa Mbunge wa Viti maalum Mkoa wa Dar es salaa, Bibi Janeth Masaburi

Mganga Mkuu wa Zahanati ya Kitunda, Bibi Judith Philipo

Waheshimiwa madiwani

Maofisa na Watendaji wote wa Sekta ya Afya

Wageni waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Habari za leo!

Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa salama na kukutanika hapa leo. Nawashukuruni wote kwa kujitokeza kwa wingi na mapokezi yenu mazuri tangu nimefika hapa. Nimefarijika sana na mapokezi yenu.

Napenda pia kuwashukuru kwa kunipa fursa ya kufika katika zahanati hii ya Kitunda. Nimefurahi kuona kuwa juhudi za dhati zimefanyika katika kuleta maendeleo katika sekta hii muhimu ya afya.

Aidha napenda niwafikishieni wingi wa salamu kutoka kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndg. Jakaya Mrisho Kikwete, anawasalimu sana na anawatakieni kila la kheri katika shughuli zenu za kila siku za kulijenga taifa letu.

Mhe. Mkuu wa Mkoa, Ndugu wananchi wenzangu
Lengo kuu la ziara yangu hapa zahanati ya Kitunda, na Mkoa wa Dar es Salaam ni kutekeleza moja ya mikakati ya Taasisi ya Wanawake na Maendeleo WAMA.
Katika Taasisi yetu tumejiwekea utaratibu wa kutembelea Mikoa yote hapa nchini ili kukutana na wananchi na hatimaye kutoa

mchango wetu katika juhudi za kuboresha afya ya uzazi ikiwemo kupunguza vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi, kuongeza ushawishi katika kuongeza fursa za Elimu kwa watoto wa kike kwa kuzungumzia changamoto za matukio ya utoro na ujauzito kwa Wanafunzi, kuchangia katika juhudi za kuwajengea uwezo Wanawake, na kuwasaidia watoto yatima.

Mhe. Mkuu wa Mkoa, Ndugu wananchi wenzangu

Tunatambua kuwa jamii yetu inahitaji huduma muhimu za afya pamoja na Elimu ya afya kuhusu magonjwa mbalimbali. Tumekuwa tukishirikiana na wadau mbalimbali katika kutoa Elimu juu ya kuzuia maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kutoka kwa Mama kwenda kwa mtoto na kufanya kampeni juu ya saratani ya matiti na shingo ya uzazi kwa Wanawake.

WAMA tuna kampeni mbili kubwa za uboreshaji afya ya Mama na mtoto, nazo ni "*Mtoto wa mwenzio ni mwanao Mkinge na UKIMWI* na *"Mlinde mtoto ambaye hajazaliwa ili aweze kuzaliwa salama.*

Kampeni hizi ni za muhimu sana katika uwajibikaji wa wananchi na viongozi wetu katika kulinda afya ya watoto na wakina mama wajawazito.

Mhe. Mkuu wa Mkoa, Maafisa wote wa afya,

Naomba tukubaliane kuwa afya ya uzazi kwa wasichana na wakinamama, Malaria na UKIMWI bado ni changamoto katika sehemu nyingi katika nchi yetu. Juhudi za dhati zinahitajika kuhakikisha kuwa huduma na elimu inatolewa kuhusiana na maswala ya afya ya uzazi, Malaria na UKIMWI. Wananchi wengi hawaelewi umuhimu wa kwenda hospitali na kupima afya zao hasa kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI. Takwimu za mwaka 2009 zinaonesha kuwa, kasi ya maambukizi kwa hapa Dar es Salaam ni 9.3 %.

Ndugu zangu kasi hii ni kubwa sana na ya kiwango cha juu kuzidi kiwango cha mambukizi Kitaifa. Changamoto naitoa kwenu leo, tujitahidi kushusha hali hii, wote kwa pamoja tukapime ili kujua afya zetu, na kuchukua tahadhari zinazotakiwa katika kujilinda. Kwani "*DAR ES SALAAM BILA UKIMWI INAWEZEKANA". TUJITOKEZE KWENDA KUPIMA AFYA ZETU.*

Nawaomba muendelee kuweka mikakati madhubuti ambayo itaongeza uboreshaji afya ya wananchi katika Wilaya ya Ilala. Naomba mtambue kuwa wananchi wanawategemea sana katika kupata Elimu na huduma bora na muhimu za afya.

Ndugu Wananchi wezangu,

Nawasihi mshirikiane katika kutunza afya zenu. Fuateni maelekezo ya madaktari na wahudumu wenu wa afya kwani hiyo ndiyo njia ya pekee ya kujikinga na magonjwa na kuishi maisha marefu. Hakikisheni mnapima afya zenu kila wakati kwani mkigundua tatizo mapema ni rahisi kupata suluhisho.

Naomba mtambue jambo moja muhimu kwamba *"Afya bora ndio msingi wa maendeleo kwa kila binadamu". Mtu mwenye afya bora hufikiri kwa umahiri na hutenda kazi kwa bidii.*

Ndugu watumishi wa Afya, Mabibi na Mabwana,

Siku ya leo Taasisi ya WAMA imekuja kuwaungana mkono katika jitihada za kutoa huduma bora za afya ya uzazi na imewaletea vifaa vifuatavyo:

- Vitanda vya hospitali (Hospital Beds) 02
- Magodoro (Mattresses) 02
- Mashuka (Bedsheets) 04
- Kifaa cha kupimia mwenendo wa upumuaji (Stethoscope) 01
- Kifaa cha kupimia shinikizo la damu (BP Machine) 01
- Kifaa cha kuwekea vifaa vya kujifungulia (Delivery Kit) 01
- Mzani wa watoto (Infant Scale) 01

Ni matumaini yangu kuwa vifaa hivi vitatumika na kutunzwa vizuri ili viweze kusaidia na wengine kwa muda mrefu zaidi.

Nimalizie kwa kuwashukuru tena kwa ushirikiano wenu mliotuonyesha na kwa mapokezi mazuri. Tunawatakia mafanikio mema katika kazi zenu za kutoa huduma katika eneo hili la afa Mungu awabariki.

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA!